


# MBOLEA SANISI

(CHUMVI CHUMVI) NI NINI?



duducoello.com

**K**una aina mbili za mbolea: mbolea ya *kilimo hai* (asili) na *isiyokuwa ya kilimo hai* (sanisi). Mbolea ya kilimo hai zinazalishwa kutohana na vitu asilia vinazopatikana kwenye mazingira. Mbolea sanisi zinatengenezwa kwa kuchanganya kemikali na vitu visivyokuwa vya asili (visivyokuwa na uhai au asili).

**Mbolea sanisi:**

- zinatengenezwa kwenye maabara au kwa vifaa vilivyo mbali na mazingira ya shamba na kuchanganya virutubisho kama vile nitirojeni, fosfati, potasiamu, chokaa, magnesi na vingineyo katika uwiano tofauti;
- zinafanya kazi haraka kwa kutoa virutubisho muhimu kwenye udongo, ambavyo hufyonza na mimea haraka;
- zinazalishwa na kufungashwa viwandani; na
- zinahifadhiwa kwenye maghala na kusambazwa sehemu mbalimbali au wakala mbalimbali kote nchini.

Matumizi ya mbolea sanisi yanatangazwa kwa mapana na serikali za nchi za Afrika ili kuongeza uzalishaji wa mazao. Serikali nydingi zinatoa ruzuku za mbolea sanisi – kama vile NPK – kama sehemu ya mpango wa ruzuku za pembejeo.